Nyaraka za Kufanyia Kazi

06. 1k

“Elimu Iliyokamilika?” Mitazamo Juu Ya Hali ya Elimu ya Msingi Tanzania – 2005

John Benson

hakielimu

"Elimu Iliyokamilika?" Mitazamo Juu Ya Hali ya Elimu ya Msingi Tanzania – 2005

John Benson[1]

"...elimu itolewayo katika shule zetu za msingi inapaswa kuwa elimu iliyokamilika."
– Mwalimu Julius K. Nyerere juu ya Elimu ya Kujitegemea (1967)

1. Utangulizi

Tanzania, kuliko nchi nyingine yeyote duniani, imetegemea elimu ya msingi kuelimisha watu wake. Ni moja ya nchi zenye asilimia ndogo sana ya watu waliohudhuria shule za sekondari (7%) ukilinganisha na taifa lolote jingine. Katika *Elimu ya Kujitegemea*, Julius Nyerere alisema kwamba inawezekana kwa Watanzania kupata elimu iliyokamilika katika shule za msingi za taifa. Vilevile, serikali ya sasa ya Tanzania imetilia mkazo elimu ya msingi katika jaribio lake la kufanikisha *Elimu kwa Wote* (UPE) kupitia *Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi*, MMEM (2002-2006).

Utafiti huu umeangalia athari za programu hizi mbili za kirais kwenye shule za msingi za Tanzania ya leo, lakini pia umeuliza maswali mawili yanayohusiana, kwa umma wa Tanzania: (1) Je, elimu ya msingi ilikuwa elimu iliyo kamili kwa watu wazima wa Taifa? na (2) Je, elimu ya msingi itatosha kwa watoto wa Tanzania?

Kwa muda mwingi wa shughuli zangu, nimekuwa nikihusika katika elimu ya msingi, nikiwa mwalimu wa shule ya msingi au profesa ninayeandaa wanafunzi kuwa walimu wa shule za msingi. Kama wengi watakaosoma makala haya, mimi pia ni mtoto wa Tanzania, ingawa ni raia wa Marekani na nimesomea tu katika shule za Kimarekani au shule za kimataifa. Nimekuwa katika nchi hii na nilivutiwa na utambuzi wa Mwalimu J. Nyerere wa kupenda kutumikia watu wa Tanzania. Nilifurahishwa na juhudi zake za kutanguliza mahitaji ya muhimu kwa nchi yake, wakati marais wengine wengi wa Afrika wamekuwa wakifanya kazi kwa ajili ya kujitajirisha wao wenyewe. Nimerudi mara kadhaa kufanya utafiti juu ya utoaji wa huduma za msingi, hivi karibuni mwaka 1993 kwa ajili ya Shahada ya Udaktari wa Falsafa katika Jiografia, ambapo nilichunguza utoaji wa huduma ya afya katika wilaya za Arusha na Arumeru, wilaya ambazo niliishi karibu miaka yote ya utoto wangu.

Nilirudi tena katika eneo la utafiti Januari 2005 kwa ajili ya kuchunguza shule za msingi katika kata sita za wilaya hizi. Nilichagua kufanya utafiti katika maeneo mawili ya miji (kata za Levolosi na Daraja Mbili katika wilaya ya Arusha), maeneo mawili mchanganyiko (kata za Mlangarini na Musa katika wilaya ya Arumeru). Nilichagua maeneo ya utafiti kwa misingi ya matokeo ya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi ya mwaka 2004, sehemu zilipo kata hizi, na miundo ya tamaduni zao.

Katika kufanya utafiti huu, nilifuatilia siku nzima ya masomo katika shule za msingi 17 kati ya shule zote 18; nilikutana na wazazi wa shule za msingi 17 kati ya shule 18; nilishauriana na viongozi wa serikali katika vijiji vyote 18 vya Arumeru na kata mbili za Arusha mjini; na nilisaili watu wanne hadi sita katika kila kata juu ya mitazamo yao binafsi kuhusu shule katika enzi zao.

[1] Dk. John Benson alikulia Tanzania na anafundisha katika Chuo Kikuu cha Minnesota State nchini Marekani. Makala haya yanatokana na mitazamo na mawazo yake binafsi alipotembelea baadhi ya shule mkoani Arusha mwaka 2005.

Sikusaili wanafunzi wa shule za msingi kuhusu maoni yao juu ya shule zao, bali nilipata nafasi ya kujifunza jinsi hali ilivyo katika madarasa yao.

2. Nyerere – Elimu ya Kujitegemea (EK)

Elimu ya Kujitegemea inaonekana kuwa ndiyo waraka wa msingi ulioathiri mitaala ya shule za msingi Tanzania. Katika waraka huo, Mwalimu Nyerere alipendekeza dira pana kwa shule za msingi za Tanzania. Je, ni kiasi gani kimebaki cha hiyo dira sasa?

Nitatumia nukuu kutoka katika waraka huo kuonyesha yale ambayo Julius Nyerere aliyaona ni ya muhimu kuhimizwa na shule za msingi za Tanzania. Alianza kwa kusema kwamba…

> …mfumo wa elimu wa Tanzania ni lazima utilie mkazo jitihada za ushirikiano na siyo maendeleo ya mtu binafsi; ni lazima uhimize fikra za usawa na wajibu wa kutoa huduma inayoendana na ujuzi wa aina yoyote ile, iwe katika useremala, ufugaji au katika taaluma. Na hasa, elimu yetu lazima ipinge kiburi cha usomi. (uk. 7)

Katika shule zote nilizoangalia, kila darasa lilionyesha hali ya ujamaa ya Tanzania, tofauti na ubinafsi wa madarasa ya Kimarekani niliyoyazoea. Wanafunzi walianza siku kwa kusafisha shule kwa pamoja kabla ya kushiriki kwenye gwaride la asubuhi ambapo wote waliimba na kukariri kwa pamoja. Kila nilipoingia kwenye darasa, wanafunzi wote walisimama kunisalimia. Katika madarasa mengi, wanafunzi walijibu maswali ya walimu kwa pamoja. Wanafunzi walishirikiana vitabu na madawati. Kila kitu cha kila siku kilifanyika kwa pamoja. Wanafunzi, kama ambavyo wangelikuwa nyumbani, waliwaheshimu wakubwa na kuwapa huduma. Sikuweza kubeba kiti kutoka darasa moja hadi lingine bila mwanafunzi kuomba kukibeba. Huduma ilikuwa shabaha kuu ya shule kama ilivyo katika vijiji vya Tanzania. Katika kupambana na kiburi cha usomi, walimu wa Tanzania hawakuwasifia wanafunzi kama nafsi pekee bali waliomba jamii nzima kuwasifia wanafunzi kwa kuwapigia makofi kwa namna mbalimbali.

> …Ni lazima pia iwaandae vijana kwa kazi ambayo watahitajika kufanya katika jamii za Tanzania – jamii ya kijijini ambapo maendeleo hutegemea kwa kiasi kikubwa juhudi za watu katika kilimo na maendeleo ya kijiji…ni lazima izalishe wakulima bora; ni lazima pia iandae watu kwa ajili ya majukumu yao kama wafanyakazi na wananchi katika jamii huru na ya kidemokrasia; japokuwa kwa sehemu kubwa ni jamii ya kijijini… hivyo ni lazima isisitize maendeleo ya kila mwananchi katika mambo matatu; akili ya kuchunguza; uwezo wa kujifunza vitu wanavyofanya wengine na kukataa au kupokea kulingana na mahitaji yake binafsi; na kujiamini katika nafasi yake kama mtu sawa na huru katika jamii yake, ambaye anathamini wengine na anathaminiwa nao kwa anachokifanya na sio kwa anachokipata. (uk. 8)

Pamoja na nia njema ya shule za Tanzania katika kujenga ujima, huduma na usawa, sidhani kama zinawaandaa wanafunzi vya kutosha kwa jamii ya sasa. Shamba la shule sio sehemu muhimu katika mtaala. Somo la Stadi za Kazi linajaribu kuwasaidia wanafunzi kwa kuwapa chaguo za mafunzo ya kazi lakini walimu hawajafundishwa jinsi ya kulifundisha, na wala hawakupewa vifaa halisi vya kulifundisha kwa usahihi. Ingawa mtaala wa sayansi nchini Tanzania ni wa kujifunza kwa vitendo zaidi kuliko kozi za sayansi nchini Marekani, sehemu kubwa ya mtaala inawaandaa wanafunzi kwa ajili ya elimu ya sekondari. Mtaala huu haufundishi wanafunzi kuwa wakulima bora na wala hausaidii kwa ujuzi unaohitajika katika Tanzania ya sasa ya utandawazi.

Niligundua pia kwamba shule zilikuwa hazitilii mkazo mahitaji ya raia ambayo Nyerere aliona ni ya muhimu sana. Nilikatishwa tamaa kuona katika madarasa wanafunzi walikuwa hawaandaliwi kufikiri sana. Wanafunzi walinakili kile ambacho walimu walikuwa wanasema au waliandika kile

ambacho walimu waliandika ubaoni, na hawakuwahi kuitwa kutoa fikra zao na kuyachanganua katika akili zao na kwa njia hiyo kujifunza kutokana na fikra hizo. Ingawa vifaa vya kufundishia ni vichache katika kila darasa, kufundisha watoto kufikiri hakuhitaji vifaa zaidi ya hivyo vilivyokuweko katika madarasa matupu ya Tanzania – yaani kuta nne, madaftari, madawati na ubao.

Katika kukutana na watu wazima Tanzania, nilifurahishwa na jinsi majibu yao yalivyokuwa yakizingatia maswali yangu, lakini nilibaki nashangaa ni nini kimewafanya kuwa wazingativu wakati elimu yao ya msingi ilifanya machache sana kuikuza hali hiyo. Sina budi kusema kwamba niliangalia ufundishaji katika vyuo viwili vya ualimu mkoa wa Arusha (Monduli na Patandi) na niliona kwamba wanatumia mbinu za kuwawezesha wanafunzi kufikiri na hizi hatimaye zitatafsiriwa na kutumika katika madarasa ya msingi ya Tanzania.

> …elimu itolewayo katika shule zetu za msingi lazima iwe elimu iliyokamilika. Haipaswi kuendelea kuwa tu maandalizi kwa ajili ya shule ya sekondari. Badala ya shughuli za shule ya msingi kulenga katika mitihani yenye ushindani ambayo itachagua wachache ambao wataenda shule ya sekondari, ni lazima iwe na maandalizi ya maisha ambayo wengi wa watoto wataishi. (uk. 15)

Nyerere aliandika kwa mapana katika waraka huo juu ya haja ya kupambana na mkazo unaowekwa kwenye kutahini na kuingia katika shule ya sekondari kama shabaha kuu ya shule za msingi. Kwa bahati mbaya hii ilikuwa shabaha kuu katika shule zote za msingi nilizotembelea. Nilipoacha kufanya utafiti mashuleni mwisho wa muhula wa kwanza na mwanzo wa likizo ndefu ya Juni-Julai, shule hazikufungwa. Wanafunzi wote wa darasa la nne na la saba walitakiwa kuja kila siku shuleni kujiandaa na mitihani yao. Kama mwalimu mkuu mmoja alivyoniambia, "kama tusipofanya hivi, hatutakuwa na hata mmoja ambaye atafaulu." Inaonekana kwamba wanafunzi wanapaswa kujua dhana walizojifunza kwa ajili ya majaribio kutokana na kuzisoma hizo dhana darasani, lakini sidhani kama walimu, wanafunzi, au wazazi wanaona kwamba mambo ya darasani yana uhusiano na yale ya kwenye mitihani.

Walimu walikuwa na hisia tofauti katika kujadili kama mitaala ya shule za msingi inasaidia kuwaandaa wanafunzi kimaisha au kwa ajili ya shule za sekondari. Baadhi waliorodhesha mambo mengi ambayo ni ya kiutendaji katika mitaala, lakini wengi waliona hawajaandaliwa vizuri kufundisha somo la Stadi za Kazi. Mifano iliyotolewa ilihusu jinsi ambavyo walifundisha masomo ya teknolojia ya redio wakati hawakuwa na redio na wao wenyewe hawajui kukarabati redio. Kundi moja la waalimu walisema kwamba wazazi hawavutiwi na mitaala ya masomo ya vitendo, bali wanachojali ni kuwafikisha watoto wao shule za sekondari.

Niliuliza wazazi kama inawezekana kupata elimu iliyokamilika katika shule za msingi tangu walipokuwa watoto hadi leo. Baadhi walidhani ilikuwa sahihi hapo zamani kwa kuwa Mwalimu Nyerere aliandika waraka wa *Elimu ya Kujitegemea* wakati sehemu kubwa ya Tanzania ikiwa "mbumbumbu" na alihitaji watu wenye elimu yoyote kujenga Tanzania mpya. Siku hizo watu waliomaliza elimu ya msingi waliweza kupata ajira. Katika makundi niliyoongea nao, hakuna aliyedhani kuwa inawezekana kupata elimu iliyokamilika katika shule za msingi siku hizi. Baadhi ya makundi walidhani kuwa hali hiyo haijawahi kutokea. Wakati huu, ulionekana ni muhimu zaidi kuliko wakati mwingine, kuingia katika uchumi wa ujira; jambo ambalo haliwezekani bila elimu ya sekondari.

Nilipotembelea jumuiya za vijijini na mijini, kazi nilizoona watu wanafanya zilikuwa kama zile za wakati nilipokuwa mtoto nchini Tanzania – yaani biashara ndogondogo, kilimo, ufugaji – hivyo niliwauliza viongozi wa serikali za mitaa kama wanaona kuwa watoto wanahitaji kuelimishwa zaidi ya elimu ya msingi. Maafisa wote wa serikali ambao niliongea nao waliona kwamba kuna

haja ya watu katika kata au vijiji vyao kuendelea zaidi ya shule ya msingi. Ulimwengu ulikuwa umewafikia katika vijiji vyao na walihitaji shule zaidi.

> …kwa wengi wa watu wetu jambo la muhimu ni kwamba, waweze kusoma na kuandika Kiswahili kwa ufasaha, na kwamba wawe na uwezo wa kufanya hisabati, na kwamba wajue mambo ya historia, maadili, na utendaji kazi wa nchi na serikali yao, na kwamba wapate ujuzi unaohitajika katika kupata riziki zao…Lakini kikubwa zaidi ya yote ni kwamba wahitimu wetu wa shule za msingi wanapaswa kurudi, kushirikiana na kutumikia jamii walizotokea. (uk. 24)

Nilipokutana na wazazi, nilianza kwa kuwauliza ni kwa kiasi gani elimu yao imewasaidia katika maisha. Wengi wao walisema kuwa shule za msingi ziliwafundisha kusoma na kuandika, ujuzi wa kufanya mahesabu, na ziliwapa ujuzi wa ziada kuwasaidia kwa kazi za shambani. Naamini walijifunza misingi ya kusoma na kuandika, lakini leo kutokana na ukosefu wa vitabu madarasani na kutokuwepo kwa vitabu vya ziada, inaoneka kuwa wengi wanashindwa na hawajifunzi kusoma.

Hata hivyo, katika hili jambo la mwisho, watu wachache wanaamini kwamba ujuzi wanaojifunza sasa katika shule ya msingi unasaidia wanafunzi kupata maarifa yoyote muhimu yanayohitajika katika maisha. Wazazi wengi wa vijijini ambao niliongea nao hawakutaka watoto wao waishi katika jamii yao kwa kuwa hakukua na ardhi iliyobaki kuwagawia. Waliwataka watoto wao wajifunze ujuzi ambao utawapeleka mbali zaidi ya mazingira ya jamii zao; na hakuna niliyeongea naye ambaye alifikiri shule za msingi zina uwezo wa kutoa ujuzi huo. Wazazi wa mijini hawakuona kama shule zilifundisha ujuzi wowote uliohitajika katika miji. Walisema kwamba kama shule hazifundishi ukulima, wazazi wa vijijini wangeweza kuwafundisha watoto wao ujuzi huo nyumbani. Wao wenyewe wangependa shule ziwasaidie kuwafundisha watoto ujuzi unaohitajika katika miji.

Mawazo mengi ya Nyerere bado yanaathiri shule za msingi za Tanzania hadi hii leo, lakini utekelezaji wake kwa vitendo umepotezwa kwa sababu ya shauku ya wanafunzi kufaulu mitihani ili kuendelea na shule za sekondari. Shule za msingi za Tanzania zinaonekana kama "msingi" tu na sio elimu iliyokamilika. Baadhi ya watu nilioongea nao walidhani kulikuwa na wakati ambapo iliwezekana kupata elimu iliyokamilika katika shule za msingi, lakini sasa hakuna anayeamini kuwa hali hiyo inawezekana ingawa kwa watoto wengi wa Tanzania, elimu ya msingi ndio elimu pekee watakayopata.

3. Mkapa – Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi

Wizara ya Elimu na Utamaduni chini ya Rais Benjamin Mkapa, ilianzisha *Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi* (MMEM) mwaka 2002. Mpango huu ni matokeo ya vuguvugu la kimataifa la Elimu kwa Wote na mikakati ya kupunguza umaskini inayoendelea nchini Tanzania. Nilivutiwa kujua ni kwa jinsi gani mpango huu ulivyofanya kazi katika ngazi za vijiji na kata nchini Tanzania. Waraka huo una sehemu kuu nne: (1) Ongezeko la uandikishaji; (2) Kuinuwa kiwango cha ubora; (3) Kujenga uwezo (4) Kuimarisha mifumo ya taasisi. Sitaweza kuzungumzia kila moja ya maeneo haya kwa ukamilifu, lakini niliweza kubaini sehemu ambazo zilifanya kazi vizuri sana na zile ambazo zilihitaji uboreshwaji.

Sehemu ya kwanza ya makala haya inaitisha ongezeko la uandikishaji kwa kufuta ada za shule, kuajiri na kuhamasisha walimu, kujenga madarasa na nyumba za waalimu, na kusaidia watoto ambao hawako mashuleni na vijana (sikufanya uchunguzi wowote kuhusiana na programu hii ya mwisho kwa hiyo sitaiongelea). Kufutwa kwa ada za shule kulionekana waziwazi kwenye idadi ya

wanafunzi katika kila darasa. Ilionyesha tofauti kubwa katika shule zote. Kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini kutoka shule ya msingi Olturoto katika kata ya Olturoto, idadi ya wanafunzi ilipanda sana baada ya kufutwa ada za shule mwaka 2001:

SENSA YA SHULE YA MSINGI OLTUROTO (1995-2004)										
MIAKA	**1995**	**1996**	**1997**	**1998**	**1999**	**2000**	**2001**	**2002**	**2003**	**2004**
WAVULANA	283	279	266	240	245	248	292	337	416	465
WASICHANA	291	277	254	254	247	252	275	343	429	462
JUMLA	**574**	**556**	**520**	**494**	**492**	**500**	**567**	**680**	**845**	**927**

Niliwauliza baba wawili wa wanafunzi wa shule ya msingi Olturoto waniambie kuondolewa kwa ada za shule kulimaanisha nini kwao kifedha. Walipojumlisha ada ya shule na ada nyingine kwa pamoja, walipata gharama ya dola 20 za kimarekani kwa mtoto kabla ya MMEM. Sasa, akina baba hawa wanaelewa kwamba gharama za shule zimepungua hadi kufikia dola 10 za Kimarekani kwa mtoto mmoja kwa mwaka ikiwa na gharama zinazotokana na sare za shule na madaftari ya ziada. Idadi hii ambayo inaonekana kuwa ndogo kwa wengi wetu, ilikuwa ni akiba kubwa kwa familia hizi na waliona kuwa wanamudu kulipa.

Uajiri na uhamasishaji wa walimu ni kipengele ambacho MMEM haikufanikiwa kabisa. Nilipokutana na walimu katika kila moja ya hizi shule, swali langu la kwanza lilikuwa, "Ni kitu gani kinakupa furaha katika kazi hii?" Karibu mara zote sikupata jibu, hadi nilipouliza kuhusu matatizo yaliyopo katika ufundishaji. Wengi walikuwa wazi kuelezea mishahara ambayo haikukimu maisha, lakini iliwabidi waishi maisha magumu kwa kuwa matakwa ya kazi ya ualimu yaliwazuia kutafuta mapato ya ziada. Wengi waliona kwamba wasingeweza kufurahia kazi hii kwa kuwa mahitaji yao ya muhimu hayakutoshelezwa. Baadae niliuliza kama MMEM ilikuwa nafuu kwa wanafunzi au walimu. Katika shule zote, walimu waliona kwamba MMEM imesaidia wanafunzi lakini haijafanya lolote kwa walimu. Programu hii imekuwa ikionekana kama ingesaidia walimu lakini hadi sasa walimu wameona MMEM haijawafanyia chochote.

Madarasa mapya yalikuwa yanajengwa katika shule 17 kati ya 18 nilizotembelea. Nyumba za walimu zilikuwa zikijengwa taratibu angalau katika nusu ya vijiji ambavyo nilifanya utafiti, lakini ukosefu wa makazi mapya katika shule nyingi lilikuwa jambo ambalo walimu wengi walitolea mfano kuwa sababu ya kuona MMEM haijawasaidia kikamilifu.

Katika eneo la ongezeko la uandikishaji, Serikali imefanikiwa katika kuleta wanafunzi wapya na kuwajengea na kuwakarabatia madarasa, lakini haikufanikiwa katika kuajiri walimu wapya na kuboresha kazi ya walimu waliokuwepo.

Sehemu ya pili ya MMEM ilitoa rai ya kuboresha rasilimali-watu ya mfumo wa elimu na kuandaa rasilimali-vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Kipengele cha rasilimali-watu ni pamoja na kuboresha ujuzi wa kufundishia wa walimu, kuwawezesha walimu kupata mafunzo zaidi, na kuwapatia walimu msaada kutoka kwa wahudumu ili kuimarisha hali ya ufundishaji.

Ufundishaji wa darasani kwa sehemu kubwa ulifanyika kwa njia ya kukariri, kumwigiza mwalimu na kunakili maandishi kutoka ubaoni kwenda kwenye madaftari ya wanafunzi. Walimu walipata mafunzo kwa makundi, lakini wengi walisema kwamba yamegawanyika katika visehemu vidogovidogo visivyoleta maana, na kwamba havikugusia mambo muhimu waliyokuwa wanakabiliana nayo kwa muda huo – yaani jinsi ya kufundisha kozi mpya kama Stadi za Kazi na kufanya kazi na wanafunzi wengi wapya. Mwalimu mmoja wa shule ya msingi Mlangarini alieleza jinsi ilivyokuwa vigumu kwao kama walimu wa vijijini kuboresha maarifa na ujuzi wa kufundisha.

Kipengele kidogo cha pili kilitoa rai ya shule kupewa vitabu na vifaa zaidi kupitia programu za kupeleka kwenye serikali za mitaa, kutoa vifaa vya kutosha kwa kila darasa, na kujenga madarasa na mandhari yaliyoboresha mafunzo. Sikuona vifaa vya ziada vya kujisomea katika darasa lolote la shule nilizotembelea, na katika shule nyingi wazazi waliorodhesha vitabu na vifaa kuwa ni vya lazima. Katika kuchunguza matumizi ya vitabu madarasani, madarasa mengi niliyoangalia yalikuwa yana vitabu pungufu chini ya kitabu kimoja kwa wanafunzi wawili au watatu. Mara nyingi vitabu hivi havikusambazwa kwa usawa darasani. Katika sehemu nyingine za darasa watoto wawili au watatu walitumia kitabu kimoja kwa wakati mmoja, na sehemu nyingine wanafunzi kumi walitumia kitabu kimoja. Mara nyingi ufundishaji ulifanyika katika misingi ya kutumia sana vitabu, lakini ukosefu wa vitabu uliathiri ufundishaji. Hakukuwa na vitabu wala vifaa vya kufundishia kozi ya Stadi za Kazi.

Vielelezo vya kufundishia vimeanza kuonekana katika shule nyingi. Katika kikao kimoja na wazazi katika shule ya msingi Levolosi mnamo mwezi Februari, niliongelea jinsi ambavyo inasaidia kuweka vielelezo vya kufundishia kwa ajili ya wanafunzi kujifunzia na nikatoa mifano yangu wakati nilipokuwa mwalimu wa shule ya msingi. Niliporudi mwezi Mei, kamati ya wazazi ilikuwa imemwajiri mchoraji kuchora ramani, michoro ya mwili wa binadamu, na kanuni za hesabu katika kuta za nje za shule. Karibu robo ya shule nilizotembelea, zilikuwa na vielelezo vya kufundishia kwenye kuta zao. Katika kuongea na mchoraji mmoja, alinieleza jinsi ambavyo MMEM imemsaidia katika riziki yake.

Eneo hili la Kuinua Kiwango cha Ubora, hali ya elimu ni dhaifu kuliko maeneo yote niliyoyaona katika MMEM. Kutokana na utafiti wangu katika hizi shule, sikuona kipengele hata kimoja kilichotoa mwitikio chanya. Hili ni eneo linalohusika na maisha ya walimu na kama walivyonieleza wanaona kuwa MMEM imewaangusha. Haikuwasaidia.

Sehemu ya Kujenga Uwezo inaongelea kuhusu kuboresha mafunzo ya awali ya walimu, utawala na menejimenti ya shule, menejimenti ya fedha katika shule, na kuendeleza mifumo ya taarifa katika kuendeleza manejimenti ya elimu. Ingawa siwezi kuongelea kuhusu eneo la mwisho, nitaongelea maeneo mengine.

Kama nilivyosema awali, MMEM imekuwa ikionekana kwa walimu wengi kuwa inafanya mambo machache katika kuwahamasisha, lakini programu za mafunzo kwa walimu wapya ingawa ni fupi kuliko ilivyokuwa hapo awali, zinaonyesha kuelekea mahali pazuri. Nilifurahishwa na jinsi ambavyo katika shule za mafunzo zenye madarasa yenye mazingira kama ya madarasa ya kawaida ya shule za msingi, wakufunzi walifundisha kwa namna ambayo iliwashirikisha wakurufunzi na kuwasukuma kufikiri. Nadhani ufundishaji huu unafaa zaidi kwa tamaduni za Kitanzania kuliko njia isiyo shirikishi ambayo ilitumika zamani.

Kamati za menejimenti za shule katika kila kijiji zilishukuru kwa mafunzo waliyopata. Mwisho wa muda wangu nchini Tanzania, mke wangu na mimi tulitoa msaada katika kila shule ambapo nilifanya utafiti. Niliomba kamati zikutane na kujadili jinsi gani wangependa kutumia dola za kimarekani 50 tulizotoa. Wote walikutana na kujadili jinsi ya kuzitumia. Kila nilipotoa misaada hiyo, karibu mara zote nilikuwa na mwalimu mkuu na mwenyekiti wa kamati ya shule; pia nilipewa risiti ya akaunti ya benki ya shule. Kamati zote za menejimenti za shule zilionekana imara na menejimenti ya fedha ya shule ilikuwepo katika kila shule.

Eneo la Kujenga Uwezo, kutokana na nilivyoona na kusikia, linaonekana kuwa imara. Shukurani zilitolewa na wengi kwa mabadiliko yaliyofanywa katika eneo hili.

Eneo la mwisho la Kuimarisha Mifumo ya Taasisi linashughulikia jinsi ambavyo shule zingeongozwa kutoka serikali kuu hadi vijijini. Kazi yangu ilikuwa katika ngazi ya kijiji, kwa hivyo siwezi kusema mengi juu ya utendaji kazi katika ngazi za juu serikalini lakini nitaongelea kuhusu niliyoyasikia au niliyoyaona katika ngazi za kata na vijiji.

Katika kila kata niliyofanyia utafiti, nilianza kazi yangu na Mratibu wa Elimu Kata. Kwa kawaida nilifuatana nao katika kila shule na walinitambulisha kwa walimu wakuu. Niliwaona wote kuwa watu makini na wachapa kazi. Wengi wao walitembea kwa miguu au baiskeli katika kata zao, mbili kati ya hizo zina eneo la kilometa za mraba 150. Zaidi ya hayo, kila mmoja inabidi afanye safari nyingi kwenda na kurudi kila mwezi kwenye makao makuu ya wilaya karibu na mji wa Arusha. Kata zingine kama vile kata ya Akeri, ambayo ni ndogo kwa eneo, shule zote zilionekana kuwa na elimu yenye ubora uliolingana. Mratibu wa Elimu Kata aliguswa sana na suala la ubora wa elimu na mara nyingi aliniuliza maswali juu ya mtazamo wangu wa hizi shule.

Katika baadhi ya kata, shule zote zilitofautiana kulingana na uwezo wa walimu wakuu. Kwa mfano, mwalimu mkuu wa shule ya msingi Akeri aliongelea jinsi alivyotumia wiki ya sikukuu ya Krismasi akifanya kazi na walimu wake ili waweze kutumia njia shirikishi katika ufundishaji wao. Wengine waliboresha mazingira ya kazi ya walimu wao kwa kuhakikisha fedha zilitumika kwa busara na kwa vitu muhimu.

Katika ngazi ya kijiji, kuwepo kwa halmashauri za kijiji katika kuendesha shule kumeonekana kwa hisia tofauti. Baadhi ya shule zilikuwa na uhusiano mwingine na taasisi za serikali – kwa mfano, Nengung'u na Chuo cha Mafunzo ya Jeshi cha Monduli; Tengeru na taasisi za kilimo za serikali – na hali hii iliumiza hizi shule kwa maana kwamba vijiji mara kwa mara vilidhani taasisi husika ingetoa msaada zaidi kwa hizi shule. Kwa upande wa Nengung'u, jeshi liliisaidia kwa kutoa watumishi na nyumba kwa ajili ya walimu, lakini palikuwa na ujenzi kidogo kwa kuwa kijiji hakikufuatilia msaada kutoka halmshauri ya wilaya. Tengeru ilikuwa shule ya pili katika kijiji cha Patandi na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo alihisi kuwa ile shule nyingine ilisaidiwa zaidi na halmashauri ya kijiji kuliko shule yake. Halmashauri nyingine za wilaya zilifanya kazi kwa ukaribu zaidi na shule ili kuboresha shule hizi kama ilivyoonekana wazi katika kijiji cha Likamba katika kata ya Musa. Madarasa mengi yalijengwa toka MMEM ilipoanza kwa msaada wa kijiji.

Kwa ujumla, maeneo ambayo MMEM naona imefanikiwa zaidi ni katika kuongeza idadi ya wanafunzi madarasani, kutoa pesa za kukarabati na kujenga madarasa mapya, kuimarisha usimamizi wa karibu na kutoa mafunzo kwa wahusika, na kuunda mifumo mizuri zaidi ya fedha. Maeneo ambayo MMEM imeonekana kutofanikiwa kabisa ni yale yanayohusiana na maandalizi ya walimu kitaifa. Walimu wanajiona wamesahaulika katika mpango mzima wa MMEM. Wanaona kama hawapewi motisha na hawaoni kama serikali imezingatia mahitaji yao kwa kadri upatikanaji wa elimu unavyoongezeka. Ni jambo ambalo wao na mimi tunaamini linahitaji kuzingatiwa upya ili MMEM ifanikiwe. Kwa imani yangu binafsi, kiini cha elimu bora sio darasa jipya; bali ni mwalimu aliyeelimishwa na kusaidiwa ili awe na uwezo wa kuwawezesha wanafunzi kujifunza. Darasa jipya haliwezi kufanya hivyo, lakini mwalimu anaweza. Walimu wanapaswa kupewa kipaumbele ili kuboresha elimu.

4. Kulinganisha EK na MMEM

Wakati miaka thelathini na tano inatenganisha kuanzishwa kwa Mpango wa *Elimu ya Kujitegemea* wa Nyerere na *Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi* wa Mkapa, mipango yote miwili ina athari kubwa katika shule za Msingi za Tanzania ya leo. Nilipokuwa naandika makala haya nilibaini kwamba mengi niliyoandika juu ya *Elimu ya Kujitegemea* yalihusu mambo ya ndani ya darasa na katika eneo la shule; wakati sehemu kubwa ya *Mpango wa Maendeleo Elimu ya Msingi* ilihusu nje ya

darasa. Mtaala unaotumika bado umebeba mambo mengi ya Nyerere kuliko ulivyokuwa na alama za Mkapa.

Kuna swali moja ambalo niliwauliza wazazi na viongozi wa serikali wa vijiji nalo lilileta majadiliano mengi; hili lilihusiana na programu zote mbili, EK na MMEM. Niliuliza: "Je, shule zina nafuu sasa kuliko zilivyokuwa zamani, au zilikuwa na nafuu zamani? Kwa nini?" Vikundi saba kati ya vikundi kumi na sita vya wazazi, na madiwani watatu kati ya madiwani kumi na mbili wa halmashauri niliowauliza hili swali waliona kuwa shule zilikuwa na nafuu sasa. Wale waliosema shule zina nafuu sasa walieleza kuwa upatikanaji wa elimu umeboreshwa. Watoto wengi waliweza kuingia shule ya msingi na wengi zaidi walifaulu kuingia shule za sekondari kuliko siku za nyuma. Mtu mmoja kutoka katika shule ya msingi Loruvani (Kata ya Olturoto) aliongelea jinsi ambavyo siku za nyuma shule zilikuwa zimejaa wavulana na wale wanaotoka katika dini fulani, lakini sasa hivi wote wana uwezo wa kwenda shule. Kundi moja liliona kuwa walimu wanafundishwa vizuri zaidi sasa kuliko zamani.

Makundi matatu ya wazazi kati ya kumi na sita na madiwani wanane kati ya madiwani kumi na wawili waliamini kuwa hali ilikuwa nafuu siku za zamani. Makundi yaliyobaki (matano ya wazazi na moja la madiwani) waligawanyika katika swala hili. Maneno niliyoyasikia mara kwa mara katika shule ni kwamba mwanafunzi aliyehitimu darasa la saba alifahamu Kiingereza kidogo sana ukilinganisha na mwanafunzi wa darasa la nne wa zamani. Jambo ambalo kundi hili lilisisitiza ni kwamba ubora wa shule ulizorota kuliko ilivyokuwa zamani. Walisema walimu walikuwa na mwelekeo zaidi katika kazi yao ya ualimu na waliuona kuwa ni wito. Hakukuwa na haja ya masomo ya ziada zamani. Kulikuwa na vifaa vingi zaidi vya kufundishia katika kila darasa. Wahitimu wa elimu ya msingi walipata ajira walipomaliza shule. Kundi moja liliongelea kuhusu heshima na mahusiano mazuri waliyokuwa nayo walimu katika jamii huko zamani. Idadi ya watoto darasani katika shule za siku hizi ilionekana kuwa ni kikwazo kinachozorotesha elimu. Yale makundi yaliyogawanyika katika suala hili hayakuwa na uhakika kama ilikuwa muhimu kupatikana kwa elimu kwa wote au kupatikana kwa elimu bora kwa walio shuleni. Haikuonekana kuwa ingewezekana kuwa na vyote viwili.

Ingawa sikuomba walinganishe elimu katika awamu hizi mbili za urais, majibu yao yalijidhihirisha. Nyerere aliongeza upatikanaji wa elimu ya msingi na wengi ambao hawakuweza kwenda kabla waliweza kuhudhuria shule, lakini sidhani kama ongezeko la idadi ya wanafunzi ilikuwa kubwa kama iliyofikiwa na MMEM. Miaka ya Nyerere upatikanaji wa elimu ulimaanisha zaidi elimu ya msingi na hiyo ilionekana kama inatosha, lakini katika miaka iliyofuatia jamii ya Watanzania imeelimika zaidi, vikwazo vya kufika sekondari vimeonekana kuwa ni hasara ya hali ya juu. Upatikanaji wa elimu ya sekondari umeongezeka katika kipindi cha Mkapa na wazazi wameliona hili kuwa ni jambo zuri.

Katika programu hizi mbili tofauti kubwa zinaonekana ni kati ya ubora dhidi ya upatikanaji. Nilipoandika kuhusu kazi ya Nyerere, uchambuzi wangu mwingi ulifanyika katika viwanja vya shule na madarasani kwa kuwa hoja yake ilikuwa ni jinsi ya kufanya mtaala uweze kuifaa Tanzania na watu wake wa vijijini. MMEM ilisema kwamba ilikuwa na nia ya kuendeleza upatikanaji wa elimu ya msingi pamoja na ubora wake. Ni kweli wanafunzi wengi wanaipata elimu na katika shule zingine madarasa yanajaa hadi kufikia watoto watano kila dawati. Karibu kila shule niliyofika kulikuwa na madarasa mapya. Menejimenti zinazorekebisha shule zimeanza. Hali ya shule kuendeshwa na jamii ya sehemu husika inaongezeka. Hata hivyo, mwenendo wa darasani ambapo ndipo ubora unaweza kupimwa sawasawa haujaguswa vya kutosha na MMEM. Walimu wanajiona kuwa wameachwa nyuma na MMEM. Mishahara yao imebaki chini, nyumba mpya zilizojengwa kwa ajili yao ni chache, na hawajapata msaada katika kufundisha maeneo mapya ya mtaala.

Ufundishaji mwingi niliouona ulikuwa wa hadhi ya chini. Wazazi wanaojali kuhusu ubora na wenye uwezo wanawahamishia watoto wao katika shule binafsi zinazotumia Kiingereza kufundishia. Ninaishi Marekani kwenye eneo lenye shule binafsi chache sana kwa kuwa watu wa eneo hilo wanaona mfumo wa shule za umma ndiyo wenye hadhi ya juu. MMEM inasema kwamba inataka shule za Serikali ya Tanzania ziwe za hadhi ya juu lakini imefanya machache kusaidia utendaji kazi katika madarasa ili kufanikisha hali hiyo.

5. Hitimisho

Nimeuliza maswali kadhaa mwanzo wa makala haya. Maswali yangu mawili ya kwanza yalikuwa yanahusu umuhimu wa elimu ya msingi kwa watu wazima wa taifa hili na kama elimu ya msingi imeonekana kuwa ya kutosha kwa watoto wa leo. Jibu la haya maswali mawili kutoka kwa watu nilioongea nao ni kwamba elimu ya msingi haikuwatosha watu wa Tanzania, na sasa, kuliko wakati mwingine wo wote, wachache wameona kuwa haitoi chochote zaidi ya elimu ya msingi.

Sehemu ya utafiti iliyobaki ilihusika na athari za *Elimu ya Kujitegemea* ya Nyerere iliyoendelea kuwepo katika shule za msingi hadi sasa na kwa kadri gani utendaji kazi wa MMEM ulivyofanikiwa. Programu ya Nyerere inaendelea kuathiri elimu ya msingi ya Tanzania. Baadhi ya maeneo ya programu yake yanaonekana katika shule za sasa, lakini kwa mengine ni kumbukumbu tu zimebaki. Mtaala siyo wa vitendo kama ulivyokuwa zamani na kuna mkazo zaidi katika kupeleka wanafunzi shule za sekondari na mkazo kidogo katika shule kutoa elimu iliyo kamili.

MMEM imefanikiwa katika kuongeza idadi ya wanafunzi shuleni na kuipa jamii nafasi ya kushiriki katika manejimenti za shule. Lakini imewatelekeza walimu, jambo ambalo limeathiri ubora wa elimu. Watanzania wengi walifurahishwa na madarasa mapya yaliyojengwa katika kipindi cha miaka michache iliyopita, lakini ni wachache walioona kuwa watoto wao wanapata elimu bora. Kwa maoni yao, walihitaji zaidi walimu imara na wanaopata ushirikiano wa wadau wa elimu kuliko majengo mapya.

Huu ulikuwa ni wakati wa kusisimua kufanya utafiti juu ya elimu nchini Tanzania. Watanzania nilioongea nao walikuwa na msisimko na walifuatilia mwelekeo wa elimu nchini. Elimu waliiona kuwa ni njia pekee ya watoto wao kufanikiwa katika Tanzania mpya ambayo inatoka kijijini kuingia duniani.

Rejea

Government of the United Republic of Tanzania, Basic Education Development Committee. *Education Sector Development Programme: Primary Education Development Plan (2002-2006).* 2001. [Accessed at http://www.tanedu.org/].

Nyerere, Julius. *Education for Self-Reliance (1967)* in *Nyerere on Education/Nyerere kuhusu Elimu*, Elieshi Lema, Marjorie Mbilinyi and Rakesh Rajani (editors), HakiElimu and E&D Ltd, Dar es Salaam, 2004

HakiElimu

HakiElimu inafanya kazi kuleta usawa, ubora, haki za binadamu na demokrasia katika Elimu, kwa kuziwezesha jamii kubadilisha mifumo ya uendeshaji wa shule, kuwa na ushawishi katika utayarishaji wa sera, kuhamasisha majadiliano ya kibunifu ya umma kwa lengo la kujiunga pamoja kuleta mabadiliko, kuendesha tafiti zinazohoji na kuchambua mambo kwa kina, kuendesha kampeni za utetezi na kushirikiana na wabia wengine ili kufikia malengo ya pamoja na kupigania haki ya jamii.

Mlolongo wa Nyaraka za Kufanyia Kazi

HakiElimu imeanzisha Mlolongo wa Nyaraka za Kufanyia Kazi (Working Paper Series) kwa lengo la kuchapisha upya makala mbalimbali za uchambuzi katika muundo ambao ni rahisi kuwafikia na kusomwa na watu wengi. Mlolongo wa nyaraka hizi unatarajiwa kuchangia katika kujenga ufahamu wa jamii na katika mdahalo kuhusu masuala ya elimu na demokrasia.

Mlolongo huu unajumuisha taarifa na makala mbalimbali zilizoandikwa na wafanyakazi na wanachama wa HakiElimu, mashirika na watu binafsi waliokuwa na ubia nasi. Baadhi ya nyaraka hizi zimeandikwa mahsusi kwa ajili ya mlolongo huu, wakati nyingine zinatokana na kazi zilizokwisha chapishwa hapo awali. Nyaraka nyingi zilizochapishwa katika mlolongo huu ni makala ambazo uandishi wake bado unaendelea, hivyo hazikukusudiwa kuwa ni nyaraka zilizokamilika kabisa.

Maoni yanayotolewa humu ni ya mwandishi (waandishi) mwenyewe na si lazima yawe yanawasilisha maoni ya HakiElimu au taasisi nyingine yoyote. Mawasiliano yote kuhusu makala mahsusi katika mlolongo huu yafanywe moja kwa moja kwa waandishi wake; kwa kadiri inavyowezekana, anuani zao zimeonyeshwa katika tanbihi/rejea chini ya ukurasa wa 1 wa makala husika.

Nyaraka hizi zinaweza pia kupatikana katika tovuti ya HakiElimu: www.hakielimu.org. Nyaraka zote zinaweza kuchapishwa kwa minajili isiyo ya kibiashara baada ya kupata idhini ya maandishi kutoka kwa HakiElimu na mwandishi husika.

Lengo letu ni kuchapisha makala fupi zilizo wazi na bayana na tungependelea zaidi ziwe na urefu wa kati ya kurasa sita hadi kumi na mbili. Hata hivyo, makala zenye urefu wa hadi kurasa ishirini zinaweza kufikiriwa. Tunakaribisha sana makala zenu. Makala hizo ziwasilishwe kwetu zikiwa katika mfumo wa kielektroniki kwa kutumia anuani inayoonyeshwa hapo chini:

HakiElimu Working Papers
PO Box 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
Tel. (255 22) 2151852 / 3 • Fax (255 22) 2152449
info@hakielimu.org • www.hakielimu.org